# Omba

**Nawezaje kuhusika? Naanzia wapi?**

Matarajio ya kuhusika na matendo ya haki ya jamii yanaweza kuonekana kuwa ya kutisha, na kiwango cha haki kinatuzidi wakati fulani. Lakini kila mmoja wetu anaweza kuomba ili kutambua hitaji na kuthibitisha jibu letu. Katika nafasi ya ukimya na ya faragha au kwenye kusanyiko la marafiki, fanya maombi yako:

*Mungu Mtakatifu na mwenye Haki,*
*nisukume nipende sawasawa.*

Niwe na nafasi kwa ajili ya maumivu ya wengine, nitoe huruma, nibebe wema wako, nitoe tumaini na uponyaji.

Nionyeshe mahali pangu na kusudi langu katika mapambano haya ya haki kwa wanawake na wasichana duniani kote na unisaidie niwe mwaminifu kuyatimiza. *Amina*

Meja Sandra Pawar, Teritori ya Marekani Kusini

**Pakua** upate misaada ya bure na mwongozo wa maombi:



HUDUMA ZA WANAWAKE
MAKAO MAKUU

JESHI LA WOKOVU

*'Jifunze kufanya vema.*
*Tafuta haki.*
*Wasaidie wanaokandamizwa.'*

(Isaya 1:17)

UNGANA NA JAMII YETU DUNIANI-KUBADILISHA WANAWAKE:

Salvation Army Women

@salvationarmywomen

https://sar.my/wm

# Tunatoa Sauti ya Vita

*kwa wanawake na wasichana!*



TUNAJITAHIDI KUIBADILISHA DUNIA kwa wema, katika jina la Mungu, tunaamini tunaweza. Kama wafuasi wa Yesu, tumeitwa kuwa chumvi na nuru katika jamii zetu, tukileta tumaini na uponyaji mahali palipobomoka. Tunaona Jeshi la wanawake wa umri wote wakiinuka kukabiliana na changamoto, wakishiriki katika kutafuta haki ya jamii na matendo ili kuigusa dunia sawasawa!

# Ilivyoanza…



**Huko nyuma mwaka 1884**, palikuwa na mawazo makubwa yaliyokuwa yakichomoza katika nia na moyo wa Florence Booth. Kama mkazi wa Mwisho wa Mashariki ya London, hali watu maelfu walikuwa wanaishi katika mazingira ya kukata tamaa, alishuhudia wanawake wengi na watoto wakihangaika kukabiliana na magonjwa, unyonyaji, kazi zisizokuwa za haki na umaskini. Ilikuwa ni lazima kufanya kitu.

Na kwa hiyo, Kazi ya Wanawake ya Jamii ilizaliwa! Wakati huo, mwaka 1907, Chama cha Wanawake kilijitokeza kutokana na maono mapya kuelekea katika namna atakavyoyowatumikia wanawake wa kizazi chake.

Florence Booth aliona hitaji naye akalijibu! Mbinu yake ya ujasiri, ubunifu, imani katika matendo inaendelea kuwahamasisha wanawake wa Jeshi la Wokovu leo.



# …Jinsi inavyoendelea!

*‘Tunapoangalia huduma ya wanawake ndani ya Jeshi la Wokovu, hatutarajii chochote kilicho chini ya wanawake waaminifu ambao kimatendo wanajibu kwa neema asilia mahitaji ya wale walio wazunguka.’*

**KAMISHENA BRONWYN BUCKINGHAM**
**Raisi wa Vyama vya Wanawake Duniani**

Zaidi ya miaka 130 baadaye, wanawake wa Jeshi la Wokovu bado wanatafuta kuibadilisha dunia kuwa njema! Kama wanafunzi, tumeitwa twende duniani tuidhihirishe habari njema ya Yesu Kristo kwa maneno na matendo. ‘Sauti yetu ya Vita’ inapazwa kwa upendo kwake Mungu na upendo kwa wengine. Tunaamini kwamba wanawake mara nyingi wamewekwa mahali pa kipekee pa kujibu kuhusu haki ya jamii. Kwa pamoja, tunauelewa wa kina wa hali nyingi na jamii, pamoja na uwezo maalum wa kutambua na kuwafariji walio katika uhitaji. Tunataka kuona Jeshi la Wokovu ambalo huwawezesha wanawake wake kwenda na kufanya jambo maridadi kuhusu ukosefu wa haki.

Sehemu nzuri zaidi? Kila mmoja ana wajibu wa kufanya – bila kujali swala ni kubwa au dogo kiasi gani, bila kujali tendo ni rasmi au sio rasmi. Moyo wako wa kutafuta haki unaweza kukufanya ujione unavuka mipaka, lakini kuishi kwa haki vinalingana – kama sio zaidi – kuhusu kutumia nguvu zako na ushawishi kwa ajili ya kuwagusa wengine katika kiwango cha mahali ulipo.

*‘Kila mmoja ana jukumu la kufanya’*

# Namna ya kushiriki

**Inafananaje kufanya mazoezi ya kuishi kwa haki?**
Kuna maelfu ya mifano ya ubunifu, ya msaada wa majibu ya haki ya jamii kote katika Jeshi la Wokovu.
*Uhamasishwe!*

*Marekani*, Lucy* anakabiliana na kipindi cha umaskini (ukosefu wa upatikanaji wa vifaa vya usafi wa hedhi menstrual) upotevu wa vifaa usiohitajika kwa kuwa mshirika wa mkondo na maduka katika eneo wanaotaka kupakua bidhaa zao za ziada za usafi wa wanawake.

Kukabiliana na ukatili wa jinsia *huko Bangladesh*, Nahida* ni mwenyeji wa klabu inayotoa masomo ya ushiriki kuhusu ridhaa, uhuru wa mwili na usafi wa mtu binafsi kwa vijana walio katika mazingira hatarishi wanaoishi katika jamii zisizo rasmi. Kwa wavulana darasa la kuwa mwanaume sahihi hufundishwa.

Wanawake wa Jeshi la Wokovu wanawalea watu katika kila umri na kila hatua ya maisha. Kutoka katika kuwatetea wanawake *huko Kenya* hadi katika kuwatia moyo akina mama wanaojifungua mtoto kwa mara ya kwanza katika kundi la wenye watoto wapya huko Uingereza, tumejitoa kuboresha maisha ya watu wote mahali pote.

***Majina yalibadilika kwa ajili ya faragha.**



**Pakua** upate hadithi za wanawake wanaoleta mguso katika kona yao ndogo duniani.